

TANGAZO

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwatangazia watu wote wanaotaka kufanya Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) mwezi **Oktoba, 2012** kama watahiniwa wa kujitegemea kwamba kipindi cha usajili kimeanza rasmi tarehe **01 Januari, 2012** kwa ada ya shilingi **35,000/=**. Kipindi cha malipo bila adhabu kinaishia tarehe **28 Februari, 2012**. Kuanzia tarehe **01 Machi, 2012** hadi tarehe **31 Machi, 2012** waombaji watajisajili kwa ada ya shilingi **50,000/=** (pamoja na faini).

Waombaji wote watajisajili kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya: **www.necta.go.tz** ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Kabla ya kujisajili kwenye mtandao waombaji watapaswa kwenda kwenye vituo vya mitihani kuchukua namba rejea (reference number) watakazotumia kujisajili. Hakuna mtahiniwa atakayeweza kujisajili bila kupata namba rejea kutoka katika kituo anachokusudia kufanyia mtihani. Wakuu wote wa vituo vya watahiniwa wa kujitegemea nchini wamekabidhiwa namba rejea hizo tayari kwa kuzigawa kwa watahiniwa tarajali **bila malipo**.

IMETOLEWA NA:

KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA